

**MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI APRILI, 2021 NA MWELEKEO  
KWA MWEZI MEI, 2021**

Dondoo za tathmini ya Aprili, 2021 na mwelekeo wa Mei, 2021:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Aprili, 2021 na mwelekeo wa viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Mei, 2021 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021 maeneo mengi ya nchi yalipata vipindi vya mvua.
- Maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata vipindi vya mvua kubwa. Aidha, maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka yaliendelea kupata mvua kuelekea mwisho wa msimu.
- Katika kipindi cha mwezi Mei, 2021 baadhi ya maeneo nchini yanatarajiwa kuendelea kupata mvua. Hata hivyo, upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi hususan yanayopata mvua mara moja kwa mwaka.

**1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2021.**

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu Kaskazini mashariki Pamoja na Pwani ya Kaskazini). Hata hivyo, vipindi vifupi vya mvua kubwa vilijitokeza pia kwa baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan magharibi mwa nchi, pwani ya Kusini na nyanda za juu Kusini magharibi. Hali hii ilisababishwa na kuimarika kwa Ukandamvua wa Kitropiki (ITCZ) katika eneo la kaskazini mwa nchi. Mnamo tarehe 7 Aprili, 2021 kituo cha Lyamungo kilichopo Kilimanjaro kilipima milimita 104.4 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi cha mvua kilichopimwa kwa mwezi Aprili, 2021 na milimita 91.4 kilichopimwa tarehe 21 Aprili, 2021 katika kituo hicho. Vituo vingine vilivyopima mvua kubwa ni pamoja na Moshi milimita 77 (tarehe 20 Aprili, 2021), Tabora milimita 68.9 (tarehe 25 Aprili, 2021), Kilwa

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd  
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

727B -00/2020

milimita 65.7 (tarehe 3 Aprili, 2021), Pemba milimita 64.9 (tarehe 8 Aprili, 2021), Songwe milimita 62 (tarehe 27 Aprili, 2021) na Musoma milimita 59 (tarehe 24 Aprili, 2021). Hata hivyo, hali ya joto katika maeneo mengi ilikuwa ya wastani hii ni kutokana na maeneo mengi kupata vipindi vya mvua na hivyo kupunguza joto.

### 2.0 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MEI, 2021

#### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifikasi inatarajiwa kuendelea kuwa la wastani hadi chini ya wastani katika kipindi cha mwezi Mei, 2021. Aidha, joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza upopo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani. Migandamizo mikubwa ya hewa kusini mwa Afrika inatarajiwa kuendelea kuimarika, hivyo kusababisha Ukandamvua wa Kitropiki (ITCZ) kusogea kuelekea kaskazini zaidi mwa nchi yetu. Hali ya joto la wastani hadi chini kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kusababisha upopo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuvuma kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

#### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2021

Mvua zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo nchini hususan wiki mbili za mwanzo za mwezi Aprili, 2021. Aidha, maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu yanatarajiwa kupata kupata mvua chache katika mwezi Mei wakati kwa maeneo yanayopata mvua za Masika upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza kuelekea

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

727B -00/2020

mwisho wa msimu wa mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini kwa mwezi Mei, 2021;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2021 hususan wiki mbili za mwanzo za Mei, 2021. Hata, hivyo upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2021.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2021 hususan wiki ya kwanza ya Mei, 2021. Hata hivyo, upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika kipindi kilichosalia cha mwezi Mei, 2021.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Mei, 2021 hususan wiki ya kwanza hadi ya tatu ya mwezi ikifuatiwa na upungufu katika wiki ya nne ya mwezi Mei, 2021.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Mei, 2021 hususan wiki ya kwanza hadi ya tatu ya mwezi ikifuatiwa na upungufu katika wiki ya nne ya mwezi Mei, 2021.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

727B -00/2020

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Katika mwezi Mei, 2021, vipindi vya ukavu vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Katika mwezi Mei, 2021, vipindi vya ukavu vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika maeneo mengi. Hata hivyo, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika wiki ya kwanza ya Mei, 2021 hususan kwa maeneo ya miinuko.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Mei, 2021 hususan wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi.

**2.3 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA MWEZI JUNI, 2021**

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2021 vipindi vya ukavu vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, hali ya joto inatarajiwa kuwa ya wastani katika maeneo mengi.

**2.4 USHAURI**

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Mei 2021 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

727B -00/2020